# Global Schools Program




# Muhtasari wa Kozi

## Darasa la 6

**Chanzo:** Reimers, F. (2017). *Empowering students to improve the world in sixty lessons*. 1st ed. Createspace Independent Publishing Platform.

**Haki Miliki:** © 2017 Fernando M. Reimers. Kazi hii imeidhinishwa chini ya leseni ya kimataifa ya Creative Commons Attribution 4.0. Kutazama nakala ya leseni hii tembelea, https://creativecommons.org/licenses/by/4.0/ Haki zote zimehifadhiwa.

**Taarifa:** Maudhui yote yaliyomo humu yameandaliwa na kuchapishwa na Programu ya Shule za Kimataifa (Global Schools Program).

SUSTAINABLE DEVELOPMENT GOALS
17 GOALS TO TRANSFORM OUR WORLD

Global Schools Program

| Muhtasari | |
|---|---|
| **Lengo la Kujifunza** | |
| Katika madarasa yaliyopita, wanafunzi walifunza maana ya kuwa sehemu ya jumuiya, walibainisha namna wanavyoweza kuchangia ustawi wa jumuiya hiyo, walijifunza kuhusu thamani ya utofauti ndani ya jamii, na kupata ujuzi wa kushirikiana na watu katika tofauti zao. Katika darasa la 6, wanafunzi watatumia lenzi muhimu kuelekea dhana hizi za jumuiya na kuanza kuchunguza jinsi fursa, ukosefu wa usawa, tofauti za uwezo, na haki ya kijamii vinavyoathiri maisha yao. | |
| **Nguzo za Somo** | |
| **Somo la 1** | Utambulisho binafsi, Fursa, na Ukosefu wa Usawa |
| **Somo la 2** | Nafasi yangu katika jamii |
| **Somo la 3** | Nafasi yangu katika taifa |
| **Somo la 4** | Nafasi yangu ulimwenguni |
| **Somo la 5** | Kufanya mabadiliko katika maisha yangu ya kila siku |
| **Madhumuni ya Kujifunza** | |
| • Wanafunzi watachunguza vipengele mbalimbali vya fursa walizonazo wao na fursa walizonazo wengine.<br>• Wanafunzi watabainisha mambo ya kihistoria, kijamii, au kiutamaduni ambayo yanaweza kuwa yamesababisha kuwepo kwa fursa hizo.<br>• Wanafunzi wataelewa jinsi utambulisho, fursa, na uzoefu wa wengine hutofautiana na wao wenyewe, na kuchukua hatua za kushughulikia ukosefu wa usawa katika maisha yao wenyewe. | |

**Darasa la 6 Somo la 1**

"Utambulisho binafsi, Fursa, na Ukosefu wa Usawa"

**Muda:** Dakika: 60
**Somo:** Insia, Maarifa ya Jamii
**Viwango:** Kukomesha Umasikini (SDG 1); Elimu ya Kiwango cha Juu (SDG 4); Usawa wa Kijinsia (SDG 5); Kupunguza kutokuwepo kwa Usawa (SDG 10); Kazi Bora na Ukuaji wa Uchumi (SDG 8); Amani, Haki na Taasisi thabiti (SDG 16)
**Imebuniwa na:** Somoh Supharukchinda (pamoja na Alexandra Ball, Deaweh Benson, Heer Shaikh, na Nicolas Riveros)

**Muhtasari na Mantiki:**

- Somo hili linalenga kuwasaidia wanafunzi kujadili na kutafakari juu ya utambulisho wao binafsi na mambo ambayo yanaunda utambulisho wao. Wanafunzi wataanza kuzingatia jinsi utambulisho wao unavyoweza kutofautiana na wa watu wengine na namna ambazo vipengele vya utambulisho vinaweza kuleta ukosefu wa usawa na/au kuwapa watu fulani fursa za upendeleo.
- Mazoezi mawili muhimu yatakuwa kama chanzo cha mjadala na tafakari:
    - Katika zoezi la kwanza, wanafunzi watashiriki katika igizo linalooonesha jinsi nafasi ya mtu inavyoweza kuathiri fursa na mafanikio yao katika maisha.
    - Katika zoezi la pili, wanafunzi watauchunguza utambulisho wao kwa kuunda "gurudumu la utambulisho" na kuoanisha jinsi vipengele vya utambulisho wao vinaweza kuathiri fursa na nafasi zao katika jamii.

**Malengo ya Ufundishaji:**

- **Ufahamu na Ujuzi:**
    - Wanafunzi kuelewa utambulisho wao na asili yao, utambulisho na asili ya wengine, namna tamaduni zinavyojenga utambulisho, na mahali ambapo mtu anaendana na mabadiliko ya wakati na mazingira (kujitambua).
    - Kuelewa jinsi maadili yanavyoundwa kupitia utamaduni, dini, na uzoefu
    - Wanafunzi wataweza kuhoji miundo ya madaraka iliyopo na kufahamu nafasi zao ndani ya muktadha mahususi wa ulimwengu

- **Mwelekeo wa Kimaadili na Kitamaduni:**
    - Kukuza kuthamini, kudadisi, na kuheshima tofauti za kiutamaduni na tamaduni za ulimwenguni kama msingi wa kujitafakari na mtazamo wa kuridhia mwingiliano wa wanadamu.

    - Imani ya usawa wa kimsingi wa watu wote na uwezo wao

**Malengo ya Uelewa:**

- Asili yangu na uzoefu hutengeneza utambulisho wangu, pamoja na fursa ambazo ninaweza kuzifikia/kuzipata.
- Asili na uzoefu wa wengine hutofautiana, na baadhi ya tofauti hizi zinaweza kuleta ukosefu wa usawa na kuathiri kiwango changu cha fursa duniani..

**Maswali Muhimu:**

- Ni mambo gani yanayounda utambulisho wetu na wa wengine?
- Je, vipengele mbalimbali vinavyounda utambulisho wetu vinaathiri vipi fursa tunazoweza kuzifikia?
- Je, tofauti hizi ni za haki? Kwa nini ndio au kwa nini sio?

**Malengo ya Mwanafunzi kujifunza (Wanafunzi wataweza):**

- Kueleza vipengele vikuu vya utambulisho wao.
- Kueleza namna vipengele vinavyounda utambulisho wao vinavyoweza kutofautiana na vya wengine.
- Kueleza jinsi utambulisho unavyoweza kuathiri fursa ambazo watu wanaweza kupata na ni upendeleo gani unaweza kuwawezesha au kutokuwawezesha kupata fursa hizo.

**Tathmini (Kazi ya nyumbani ya hiyari):** Wanafunzi wataandika nukuu fupi juu ya tafakari zao kutoka kwenye mazoezi ya utambulisho binafsi na kushirikisha mifano miwili wanayoona ya jinsi tofauti za utambulisho zinavyoweza kuathiri fursa ambazo wao au wengine wanaweza kuzifikia..

**Mpangilio wa Mazoezi:**

- **Kutambulisha Somo (Dakika: 1):**
    - Eleza wanafunzi kwamba madhumuni ya somo ni kuchunguza utambulisho wao, ni nini kinachounda utambulisho wao, jinsi wanafunzi wanavyoweza kutofautiana na wengine, na jinsi utofauti huu unavyoathiri fursa wanazoweza kuzifikia. Ikiwa wanafunzi hawaelewi msamiati huu, fafanua utambulisho kuwa ni namna “unavyojifafanua kwa watu."

- **Fanya zoezi la ukosefu wa usawa (Dakika: 9):**
    - Wanafunzi wanapoingia darasani, wanapangiwa viti. Kila kiti kina karatasi iliyokunjwa.

  - Waelekeze wanafunzi kuwa wana nafasi ya kushinda tuzo. Ili kushinda tuzo, wanapaswa kubaki kwenye viti vyao na kutupa karatasi zao kwenye "kikapu" (kopo la takataka) mbele ya chumba cha darasa.
  - Wanafunzi wanapaswa kuketi ili baadhi ya viti viwe na nafasi za mbele kwenye urahisi wa kufikia kikapu. Wanafunzi watakaoweza kutupia karatasi zao katika kikapu watapokea zawadi (k.m. peremende, chokoleti, n.k.). Wanafunzi watakaoweza kutupia karatasi zao kwenye kikapu wanaweza kupewa karatasi zingine zilizokunjwa ili kupata nafasi zaidi za kushinda zawadi.

- **Ongoza Muhtasari/Majadiliano (Dakika: 14):**
  - Acha wanafunzi wajadili idadi ya zawadi walizopata, nani alipata zawadi, na jinsi walivyojisikia. Iwapo wanafunzi hawaoneshi hisia zozote za kufadhaika au kukwazika, wahimize kujadili ikiwa waliona zoezi hili liliendeshwa kwa haki. Je, wanafunzi waliokuwa mbele wangeweza kuwasaidia wanafunzi waliokuwa nyuma (kwa mfano, kwa kuwagawia karatasi zao za ziada)?
  - Washirikishe wanafunzi kuwa zoezi hili lilikusudia kuonesha tofauti zilizopo katika maisha halisi. Je, wanaona uhusiano gani kati ya zoezi hili na maisha halisi? Je, ikiwa pipi zilikuwa pesa, shule, kazi, nk. Ni mambo gani katika maisha halisi yanaweza kusababisha mtu kujikuta amekaa kiti cha mstari wa mbele badala ya safu ya nyuma?

- **Fanya zoezi la gurudumu la utambulisho (Dakika: 18):**
  - Washirikishe wanafunzi kwamba darasa sasa litashiriki katika zoezi linalowaruhusu kuchunguza kwa kina zaidi maswali ya utambulisho. Kwanza, utatengeneza gurudumu la utambulisho kama mchoro wa duara lenye sehemu zinazowakilisha kila kipengele cha utambulisho wako - kwa mfano, jina, jinsi, rangi, nafasi katika familia yako, n.k. Ukubwa wa sehemu za duara unapaswa kuendana na kiasi ambacho kipengele hicho kinachangia kujenga utambulisho wako (vipande vikubwa vinamaanisha kuwa kipengele hicho ni sehemu kubwa ya utambulisho wako). Washirikishe wanafunzi kwa nini ulichagua vipengele ulivyochagua na kwa nini ulivipa ukubwa kama ulivyofanya?
  - Waagize wanafunzi kuunda gurudumu lao la utambulisho kulingana na kile wanachofikiria ni muhimu kwenye utambulisho wao. Kila mmoja wao anapaswa kuwa na kipande cha karatasi na kalamu ya rangi/penseli za rangi za kuchorea/vifaa vya kuandikia. Unaweza kuwahimiza kuzingatia:
    - Jiografia (Nchi, Mji, kijiji, nk.)
    - Jinsi
    - Rangi/jadi/kabila/nk.

        - Dini
        - Mahusiano ya Kifamilia (binti, kijana, kaka, nk.)

- **Shirikisha na jadili magurudumu ya utambulisho (Dakika: 10)**
    - Katika vikundi vya watu 3-4, waelekeze wanafunzi washirikishane magurudumu yao ya utambulisho yaliyokamilika, wakishirikisha pia kwa nini wamechagua vipengele walivyovichagua  na ukubwa wa vipengele walivyovichagua.

- **Hitimisho (Dakika: 8)**
    - Acha wanafunzi wawasilishe:
        - Ni utambulisho gani waliufahamu zaidi?
        - Je, walifikiria kuhusu aina nyingine za utambulisho?
        - Je, aina hizo za utambulisho zilikuwa tofauti na za wanafunzi wenzao?
        - Je, walishangazwa na chochote walichokiona kwenye magurudumu ya utambulisho wa wanafunzi wenzao? Kwa nini walishangazwa au kwa nini hawakushangazwa?
        - Je, haya yanaweza kuhusiana vipi na zoezi la kwanza?

**Nyenzo kwa ajili ya walimu:**
- https://www.recipesforwellbeing.org/the-wheel-of-power-and-privilege/#:~:text=The%20wheel%20of%20power%20and%20privilege%20is%20a%20reflective%20activity,by%20systems%20in%20our%20society.
- https://brendaethn21portfolios.weebly.com/reading-blog/personal-identity-wheel

**Darasa la 6 Somo la 2**

"Nafasi yangu katika Jamii"

**Muda:** Dakika: 60
**Somo:** Maarifa ya Jamii, Kiingereza, Uraia
**Viwango:** Kukomesha Umasikini (SDG 1); Kupunguza kutokuwepo kwa usawa (SDG 10); Miji na Jamii Endelevu (SDG 11); Amani, Haki na Taasisi Thabiti
**Imebuniwa na:** Alexandra Ball

**Muhtasari na Mantiki:** Katika somo hili, wanafunzi watapanua uelewa wao wa mapendeleo na utambulisho waliojifunza katika Somo la 1 katika kiwango cha jumuiya.

- Wanafunzi wataanza kwa kukumbuka magurudumu ya utambulisho waliyounda katika somo lililopita; hii itatumika kama kianzio cha mjadala mfupi wa jinsi vipengele tofauti vya utambulisho wa mtu vinavyoweza kuathiri upendeleo na fursa zao.
- Kisha, mwalimu atawaongoza wanafunzi katika uchunguzi wa jinsi ukosefu wa usawa unaweza kuathiri watu wanaoishi katika jamii moja, kwa kutumia mfano maalum wa usawa wa kipato.
- Wanafunzi wataanza jaribio la mawazo elekezi kuhusu jinsi watu wawili walio na viwango tofauti vya kipato wanaweza kuwa na maisha na uzoefu tofauti sana, licha ya kuishi katika jamii moja.
- Wanafunzi watafakari juu ya uzoefu huu kwa zoezi la kuandika kwa haraka la dakika 5, ambalo watashirikishana katika vikundi vidogo.
- Wanafunzi watatoka katika makundi na darasa litakutana tena kwa mjadala wa darasa zima ambapo wanafunzi watashirikisha mawazo yao juu ya zoezi hilo, na kujadiliana njia ambazo jamii yao inaweza kukuza usawa.

**Lengo la Ufundishaji:** Kuwaongoza wanafunzi katika jaribio la tafakari juu ya athari za ukosefu wa usawa ndani ya jamii.

**Malengo ya Uelewa:** Hata ndani ya jumuiya moja, watu wanaweza kuwa na viwango tofauti vya upendeleo, uzoefu tofauti, na uwezo tofauti. Lazima nifahamu mienendo hii inavyofanya kazi ndani ya jumuiya yangu, na nianze kufikiria jinsi usawa wa fursa unavyoweza kukuzwa katika ngazi ya mtaa.

**Maswali Muhimu:**

- Je, wanajumuiya wote wa jamii ni sawa kiotomatiki? Kwanini wako sawa au kwanini hawako sawa?

- Je, ni yapi madhara ya ukosefu wa usawa katika ngazi ya mtaa?
- Je, jumuiya zinaweza kufanya nini ili kuhakikisha kwamba watu wote wana uhuru na fursa sawa?

**Wanafunzi wataweza kufanya yafuatayo:**

- kutumia mafunzo ya awali kwa matukio ya kufikirika na maisha halisi.
- Kufikiria kwa kina juu ya kile wanachokiona katika maisha yao ya kila siku.
- Kuonesha ubunifu katika kutatua matatizo ya kijamii.

**Tathmini:** Mwishoni mwa darasa, kila mwanafunzi atawasilisha pendekezo moja la kutatua tatizo la usawa wa kipato katika ngazi ya mtaa (katika muktadha wa zoezi la darasani).

**Mpangilio wa Mazoezi:**

- **Utangulizi/Kufafanua misamiati (Dakika: 5):**
    - Utaeleza kwamba wanafunzi watakuwa wakichunguza ukosefu wa usawa kama ulivyo ndani ya jumuiya fulani. Kisha unapaswa kuuliza darasa wanafikiri jumuiya ni nini, na kwa kutumia mapendekezo ya wanafunzi, uandike ufafanuzi wa darasa kuhusu "jumuiya" ubaoni.
    - Ufafanuzi huu unaweza kuelezea mtaa, mji, kijiji, shule, au jiji; kwa jinsi utakavyoamua kwa hiyari yako.

- **Kutunga/Somo la 1 Muhtasari (Dakika: 5):**
    - Utawaelekeza wanafunzi wakumbuke ramani zao za utambulisho kutoka darasa lililopita. Kisha, utawaelekeza wanafunzi kugeukiana na kuzungumza na wanafunzi wenzao kuhusu vyanzo mbalimbali vya utambulisho tofauti ambavyo walivitambua kupitia ramani zao.
    - Unapaswa kuzunguka kwa takriban dakika tatu, kusikiliza majadiliano ya wanafunzi na kuwachochea kufikiria mambo mengi zaidi ambayo yanaweza kuunda utambulisho wa mtu.

- **Utangulizi wa Townville (Dakika: 10):**
    - Baada ya kuwakutanisha tena wanafunzi, utawatambulisha kwa "Mji mpya," jumuiya ya kubuni. Utachora ramani rahisi ya Townville ubaoni, ukibainisha vipengele kama vile shule, soko, barabara, maeneo ya katikati mwa jiji, vipengele vya kijiografia, ukumbi wa jiji, n.k.

- Kisha, utachora nyumba mbili kwenye ubao: Nyumba ya duara na nyumba ya mraba. Nyumba hizi ni majirani wa huko Townville; wote wanaishi familia yenye mama, baba na mtoto mmoja.
  - Tofauti pekee ni kwamba mapato ya kila mwaka ya nyumba ya duara ni Townbucks 100, wakati mapato ya nyumba ya mraba ni shilingi.
  - Kisha utaeleza kwamba wanafunzi wataona jinsi maisha yatakavyokuwa katika kila nyumba.

- **Kuandaa zoezi (Dakika: 5):**
  - Utaligawa darasa katika pande mbili: upande mmoja utawakilisha nyumba ya duara na nyingine itawakilisha nyumba ya mraba.
  - Ndani ya makundi haya mawili, wanafunzi wanapaswa kujigawa katika vikundi vya watu 3-4. Wanapofanya hivyo, utawapatia pesa za shilingi kwa kila kikundi: Vikundi vya nyumba ya duara vitapata shilingi 10, na vikundi vya nyumba ya mraba vitapata shilingi 5.
    - Unatakiwa kuandaa noti za kutosha kabla ya muda wa darasa.

- **Zoezi (Dakika: 10):**
  - Mara wanafunzi watakapokuwa katika vikundi na kuwa na pesa zao, utaandika mfululizo wa shughuli ubaoni, kila moja ikiwa na bei tofauti (idadi zinapaswa kuwa katika nyongeza za 10, hadi shilingi 50).
  - Mazoezi yanapaswa kuwa mazoezi ya kawaida kwa wanafunzi wa darasa la 6 katika muktadha ambamo somo linatekelezwa (yaani kubarizi na marafiki, kuchora, kusoma, n.k.)
  - Kisha utaeleza kwamba hizi shilingi zinawakilisha kiasi gani cha fedha ambacho kila mtoto alijiwekea akiba; sasa, kila kikundi kitalazimika kuamua wanataka kutumia pesa zao namna gani na kwa nini wamechagua kuzitumia namna hiyo. (uko huru kuchagua aina ya zoezi utakalowapa wanafunzi - linaweza kuwa rahisi kama orodha ya vitu, au mlolongo wa mazoezi yenye gharama ndogo).

- **Kukutana tena/Majadiliano (Dakika: 10):**
  - Baada ya dakika 10 za majadiliano ya kikundi, kwanza utauliza kila Kikundi cha nyumba ya duara walitumia vipi pesa zao, na kisha kila kikundi cha nyumba ya mraba walitumia vipi pesa zao.
  - Kisha utaongoza darasa katika mjadala wa kulinganisha namna pande zote mbili zilivyochagua kutumia pesa zao, na kuwachochea wanafunzi kujadili kama waliona kuwepo kwa usawa katika hili na kama hawakuona usawa ni kwa nini.

        - Huenda ikasaidia zaidi kuchochea majadiliano kwa kusema mambo kama, “Lakini watoto hawa walikuwa na fursa sawa na walikuwa majirani. Ni nini kisicho sawa katika hilo?"

- **Katika jumuiya yetu wenyewe (Dakika: 10):**
    - Kisha utawaelekeza wanafunzi kuchukua kipande cha karatasi na kuandika andiko huru kwa dakika 5 kuhusu jinsi zoezi hili linavyofanana na jumuiya yao.
        - Wakati huu, unapaswa kuzunguka darasani kuangalia wanachoandika wanafunzi na unaweza kuchochea wanafunzi wanaotatizika kwa maswali kama vile, "ungejisikiaje kuishi katika nyumba ya mraba?" au “Je, unaweza kufikiria njia zozote isipokuwa kipato ambazo familia katika jumuiya moja zinaweza kutofautiana?”
    - Baada ya dakika 5, unaweza kuwataka wanafunzi kuwasilisha mawazo yao.
        - Utalazimika kudhibiti mjadala huu kwa uangalifu, kwani wanafunzi watakuwa wakizungumza kuhusu jumuiya zao na wanaweza kukiuka baadhi ya mada nyeti na/au binafsi.

- **Kuhitimisha (Dakika: 5):**
    - Kama kuna muda wa kutosha, unapaswa kuwauliza wanafunzi kitu wanachofikiri kinaweza kufanywa ili kuhakikisha kwamba mtoto kutoka nyumba ya mraba anapata fursa zote sawa na mtoto kutoka kwenye nyumba ya duara.
    - Baada ya mjadala wa darasa, kila mwanafunzi anapaswa kuandika pendekezo moja, ambalo linaweza kutumika kama tiketi yao ya kutoka darasani.

**Nyenzo kwa ajili ya walimu:**
- https://www.youtube.com/watch?v=-5wo1ArN88w&t=10s
- https://www.youtube.com/watch?v=H4pI2XcCHbw
- https://www.youtube.com/watch?v=6DIQq2xLw_0&t=1s
- https://www.youtube.com/watch?v=SsrMVni1G94

**Darasa la 6 Somo la 3**

"Nafasi yangu katika taifa"

**Muda: Dakika:** 45
**Mada:** Historia, Maarifa ya Jamii, Sanaa ya Lugha
**Viwango:** Kupunguza kutokuwepo kwa Usawa (SDG 10); Amani, Haki na Taasisi thabiti (SDG 16); Ubia ili Kuyafikia Malengo (SDG 17)
**Imebuniwa na:** Alexandra Ball, Heer Shaikh, Deaweh Benson, Somoh Supharukchinda

**Muhtasari na Mantiki:**

- Katika somo hili, wanafunzi watajadili ukosefu wa usawa katika muktadha wa kitaifa, wakiwa tayari wameanza kuchunguza utambulisho wao binafsi/nafasi yao katika jamii.
    - Hasa, watasukumwa kufikiria jinsi uzoefu wao unavyolinganishwa na ule wa wengine katika nchi yao, jinsi wanavyoweza kuwa tofauti, na kwa nini.

- Hili litakamilishwa kupitia ufanyaji mazoezi ya mtindo wa uandishi/utendaji wa "chagua-zoezi lako-mwenyewe"
    - Wanafunzi "watatambulishwa" kwa watoto watatu, wote wakitoka katika jumuiya/maeneo/tamaduni tofauti ndani ya nchi yao.
    - Baada ya kupewa baadhi ya taarifa za msingi kuhusu maisha ya watoto hao, wanafunzi watagawanywa katika makundi na kutakiwa kufikiria/kuwasilisha hatua mbalimbali za maisha ya watoto hao.
    - Baada ya kuwasilisha kwa kikundi, wanafunzi wataeleza kwa ufupi jinsi uzoefu wa watoto hawa ulivyotofautiana na uzoefu wao wenyewe na sababu za tofauti hizo.

**Malengo ya Ufundishaji:**

- Kuwaongoza wanafunzi katika kufikiria maisha yangekuwaje kwa watu wengine katika muktadha wao wa kitaifa.
    - Ili kufanya somo hili litumike katika miktadha tofauti ya kitamaduni, unapaswa kuunda wasifu wa watoto watatu kabla ya somo. Wasifu huu unapaswa kuwa na maelezo ya msingi kuhusu mtoto wa kubuniwa (jina, anakotoka, familia, ikiwa anaishi katika mazingira ya mijini/vijijini, dini, au maelezo mengine yoyote ambayo yanaweza kuwa muhimu kwa zoezi hili).
    - Ili somo lifanikiwe, hata hivyo, maelezo haya lazima yawe tofauti kati ya watoto hawa.

**Lengo la Uelewa:** Hata ndani ya nchi yangu, watu wa mikoa/jamii/tamaduni mbalimbali wana uzoefu na fursa tofauti na mimi.

**Maswali Muhimu:**

- Je, uzoefu/utambulisho huu wa watu wengine ndani ya nchi yangu unatofautiana vipi na wangu?
- Je, ni sababu zipi zinazofanya uzoefu huu kutofautiana?
- Je, tofauti hizi huathiri vipi fursa/mwelekeo wetu wa maisha?

**Malengo ya Kujifunza ya Mwanafunzi (Wanafunzi wataweza kufanya yafuatayo):**

- Kusoma/kuelewa maelezo ya wahusika wao.
- Kuunda/kuwasilisha uwakilishi wa wahusika wao wakiwa na umri wa miaka 11, 16, na 21.
- Kushiriki katika mjadala wa jinsi uzoefu wa wahusika hawa katika kila umri hutofautiana, kwanini tofauti hizi zipo, na umuhimu wa tofauti hizi.

**Tathmini:**

- Ingawa hakuna tathmini rasmi, mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi anashiriki kazi ya kikundi, na kushiriki katika uwasilishaji wa hadithi ya kikundi chao.
- Kila mwanafunzi anapaswa kuwasilisha muhtasari wa sentensi moja wa kitu alichojifunza (kama tiketi ya kutoka).

**Mpangilio wa Mazoezi:**

- **Utangulizi (Dakika: 10)**
    - Wanafunzi watapewa mfano wa "hadithi" ya mwanafunzi wa kawaida kutoka katika jumuiya yao wenyewe - Utambulisho kwa mwanafunzi na maelezo mafupi ya maisha/jumuiya/familia ya mwanafunzi huyo.
    - Kisha wanafunzi huwasilishwa na wasifu mfupi wa wanafunzi watatu zaidi, kila mmoja kutoka tamaduni/maeneo/jamii mbalimbali ndani ya nchi yao, na kupewa maagizo ya kufikiria jinsi maisha ya wanafunzi hao yanaweza kutofautiana na yao wenyewe, na kwa nini.
    - Wakati wa maagizo haya, unapaswa kutoa vidokezo kama vile:
        - "Je, mwanafunzi huyu atakwenda shule namna hii?"
        - "Unafikiri mwanafunzi huyu anapenda kufanya nini ili kujifurahisha?"

- **Mpangilio wa Zoezi (Dakika: 2)**

    - Wanafunzi wagawanywe katika vikundi vya wanafunzi 4-5, kila mmoja apewe mmoja wa wanafunzi wa hadithi. Vikundi vingi vinaweza kupewa mwanafunzi mmoja.

- **Zoezi (Dakika: 10-15)**
    - Katika vikundi, wanafunzi watasimulia hadithi ya mwanafunzi wao wa kubuni. Wanafunzi wanaweza kuchagua namna ambayo wanataka kueleza hadithi yao (kwa maandishi, kuigiza, sanaa, n.k.). Unapaswa kuwa na nyenzo mbalimbali kwaajili ya wanafunzi kutumia wakitaka.

- **Wasilisho (Dakika: 10)**
    - Kila kikundi kitawasilisha mbele ya darasa hadithi ya mwanafunzi wao wa kubuni.

- **Mjadala (Dakika: 10)**
    - Baada ya wanafunzi kumaliza kuwasilisha, unapaswa kuongoza darasa katika mjadala wa jinsi hadithi zote zilivyokuwa tofauti, ingawa zote zilihusu wahusika wa kutoka nchi moja. Unapaswa basi kuwasukuma wanafunzi kuzingatia njia ambazo hadithi zilifanana.

- **Hitimisho : (Dakika 2)**
    - Kabla kipindi hakijamalizika, kila mwanafunzi anapaswa kuandika kitu kilicho mshangaza katika zoezi hili.

**Nyenzo kwa ajili ya walimu:**

- Mifano ya njia za ubunifu za kuwasilisha hadithi za watoto: https://www.mrsbrownart.com/
- https://worldslargestlesson.globalgoals.org/resource/global-goals-comic-posters/
- https://developmenteducation.ie/resource/comics-uniting-nations-heroes-for-change/
- https://developmenteducation.ie/media/documents/Heroes%20For%20Change.pdf
- https://www.canva.com/comic-strips/templates/

**Darasa la 6 Somo la 4**

"Nafasi yangu Ulimwenguni"

**Muda:** Dakika: 45
**Mada:** Jiografia, Uraia
**Viwango:** Kukomesha Umasikini (SDG 1); Elimu ya Kiwango cha Juu (SDG 4); Kupunguza kutokuwepo kwa Usawa (SDG 10); Amani, Haki, na Taasisi thabiti (SDG 16)
**Imebuniwa na:** Alexandra Ball, Heer Shaikh, Deaweh Benson, Somoh Supharukchinda

**Muhtasari na Mantiki:**

- Katika somo hili, wanafunzi wataoneshwa ukosefu wa usawa wa kimataifa ili kuongeza ufahamu wao na ukubwa na umuhimu wa jukumu lao kama raia wa kimataifa.
- Hii itaendana na mada katika mfumo wa kukuza uthamini, udadisi, na heshima kwa tofauti za kiutamaduni na utamaduni wa ulimwengu kama msingi wa kujitafakari, kuunda utambulisho, na mwingiliano wa kibinadamu wenye uelewa kwa hisia za wengine.
- Wanafunzi wanapaswa kutambua na kuthamini umuhimu wa kila mtu, viumbe hai na sayari.

**Lengo la Ufundishaji:** Somo hili litawafichulia wanafunzi takwimu za kimataifa na tofauti zake, na kuwahimiza kuzingatia wajibu wao binafsi.

**Malengo ya Uelewa:** Wanafunzi wataelewa jinsi ukosefu wa usawa katika ngazi ya kimataifa unavyoathiri jinsi nchi zinavyoingiliana, na pia watapata ujuzi muhimu wa kutatua matatizo ya jamii zao.

**Maswali Muhimu:**

- Ni nini hufanya nchi kutofautiana?
- Je, tofauti hizi huathiri vipi mwingiliano wao?
- Je, mwingiliano huu wa kimataifa unaathiri vipi maisha ya watu?

**Malengo ya Mwanafunzi kujifunza (Wanafunzi wataweza kufanya yafuatayo):**

- Kujiweka kwenye nafasi ya mtu mwingine na kufikiria kwa umakini juu ya matendo yao.
- Kufanya mazoezi ya kutatua matatizo na kushirikiana na wanafunzi wenzao.
- Kuelewa jinsi migogoro inavyotokea katika ngazi ya kimataifa.

**Tathmini:** kazi ya mwisho baada ya wanafunzi kupokea masahihisho; maoni kutoka kwa "mhariri wa gazeti" (ama mwalimu au mwanafunzi darasani).

**Mpangilio wa Mazoezi:**

- **Utangulizi (Dakika: 5)**
  - Utawauliza wanafunzi ili kuona kama wanakumbuka masomo mawili ya mwisho, ambapo walichunguza masuala ya ukosefu wa usawa na utofauti katika ngazi ya jamii na kitaifa. Kisha, utaeleza kuwa leo, wanafunzi watakuwa wakitumia masomo hayo hayo kwa kiwango cha kimataifa kupitia mfano wa Umoja wa Mataifa (UN).
  - Utaelezea kwa ufupi UN ni nini na jinsi nchi zinavyotuma wawakilishi huko kufanya mazungumzo kwa niaba ya nchi nzima. Unaweza kuwaonesha wanafunzi tovuti ya Umoja wa Mataifa au vyombo vingine vya habari kwenye Umoja wa Mataifa, ikiwa muda na nyenzo zinakuruhusu.

- **Mpangilio wa mazoezi (Dakika: 10)**
  - Utaeleza kuwa wanafunzi watakuwa wakiigiza nchi mbalimbali. Ili kufanya hivyo, unapaswa kugawa darasa katika vikundi vya wanafunzi 4-5. Kisha kila kikundi kitapewa nchi. Nchi zinapaswa kuwakilisha tofauti ya ukubwa, kanda, makabila na uchumi.
  - Mara tu vikundi vyote vitakapopewa nchi, utaunganisha tena darasa na kuwapa tatizo la kusuluhisha. Umeachwa huru kuamua aina ya tatizo utakalowapa wanafunzi kusuluhisha, lakini ingefaa zaidi kama ni jambo ambalo wanafunzi wana kiwango fulani cha ufahamu kuhusu tatizo hilo, au jambo muhimu kwa jamii ambamo somo hili linafundishwa.
    - Matatizo hayo yanaweza kujumuisha: vita kati ya nchi mbili katika chumba hicho, uhaba wa maji/rasilimali katika eneo, tatizo katika nchi nyingine, n.k.
  - Kisha unapaswa kugawa kwa kila kikundi karatasi inayoelezea msimamo wa nchi yao kuhusu tatizo (karatasi hizi zitayarishwe kabla ya kipindi). Hii inapaswa kujumuisha taarifa kuhusu maoni ya wananchi/viongozi wa nchi, wadau wowote wa kiuchumi/rasilimali wanaoguswa na tatizo linalojadiliwa, na pia nguvu ya ushawishi/mapatano yoyote ambayo nchi inayo na nchi nyingine katika igizo hilo).

- **Zoezi (Dakika: 15)**
  - Kwa kufuata maelekezo yako, wanafunzi wataingia katika vikundi vyao na kujaribu kufikia uamuzi wa maelewano kuhusu jinsi ya kutatua tatizo. Wakati huu wanafunzi wanapaswa kuachwa huru kupanga mikakati ndani ya vikundi vyao au kujadiliana na vikundi vingine.
  - Wakati huu, unapaswa kuzunguka ili kuwezesha mazungumzo kati ya wanafunzi. Unapaswa kuhakikisha kuwa vikundi vyote vinazingatia mikakati ambayo itakuwa

na manufaa kwao wenyewe na jinsi maslahi yao yanaweza kutofautiana na maslahi ya nchi nyingine.

- **Darasa kuungana tena (Dakika: 10)**
  - Utawaita darasa warudi pamoja na kuwaagiza wawasilishe kwa pamoja suluhisho lao (kama waliweza kufikia suluhisho moja).
  - Kisha utaongoza darasa katika mjadala wa zoezi, na kuwashawishi kuzungumzia:
    - Je, ilikuwa vigumu kukubaliana na nchi ambazo zilikuwa tofauti na zako? Kwa nini ilikuwa vigumu/rahisi?
    - Ulilinda vipi masilahi yako wakati wa mazungumzo?
    - Je, kuna baadhi ya nchi zilikuwa na nguvu zaidi kuliko nchi nyingine? Kwa nini?
    - Je, huu ulikuwa mchakato wa haki? Kwa nini ulikuwa wa haki au kwa nini haukuwa wa haki?

**Nyenzo:**

- http://news.bbc.co.uk/2/hi/country_profiles/
- https://www.cia.gov/the-world-factbook/
- https://unausa.org/programs/model-un/
- https://www.un.org/en/mun/model-un-guide

**Darasa la 6 Somo la 5**

"Kufanya Mabadiliko katika Maisha Yangu ya Kila Siku"

**Muda:** Dakika: 45
**Mada:** Maarifa ya Jamii, Uraia, Sanaa
**Viwango:** Komesha Umasikini (SDG 1); Elimu ya Kiwango cha Juu (SDG 4); Kupunguza kutokuwepo kwa usawa (SDG 10); Amani, Haki, na Taasisi thabiti (SDG 16)
**Imebuniwa na:** Alexandra Ball

**Muhtasari na Mantiki:**

- Katika somo hili, wanafunzi wataelekeza lengo lao kwenye ngazi ya mtaa, wakichagua tatizo wanalotaka kuunga mkono utatuzi wake ndani ya jumuiya yao.
    - Tatizo hili linaweza kuwa tatizo lolote linalogusa masilahi binafsi ya wanafunzi - ulinzi wa mazingira, njaa, ukosefu wa makazi, usawa wa rangi, n.k.
- Wakati wa somo hili, wanafunzi wataandaa orodha ya mambo matano yanayoweza kufanyika ili kutatua tatizo hili katika maisha yao ya kila siku. Kisha watatengeneza mabango ya hatua hizi tano, ambayo yataoneshwa katika shule/darasa zima.

**Malengo ya Ufundishaji:** Kutambua matatizo ya ukosefu wa usawa/uhitaji ndani ya jumuiya zao na kuwawezesha wanafunzi kuchukua hatua za binafsi kutatua matatizo yanayogusa maslahi yao binafsi.

**Malengo ya Uelewa:**

- Lazima nitazame kwa jicho la kidadisi kile ninachoona kikifanyika kila siku katika jamii yangu.
- Nina uwezo na nguvu ya kuleta mabadiliko, na nina jukumu la kujaribu kuleta mabadiliko.

**Maswali Muhimu:**

- Je, matatizo ya ukosefu wa usawa, fursa za upendeleo, na haki yanahusiana vipi na jamii yangu mwenyewe?
- Ninaweza kufanya nini ili kutatua matatizo haya katika maisha halisi?

**Malengo ya Wanafunzi kujifunza (Wanafunzi wataweza kufanya yafuatayo):**

- kutambua tatizo linalowagusa wao binafsi kwao na hitaji kubwa katika jamii.
- kuandaa orodha ya njia tano za kutatua tatizo hilo.
- kushirikisha orodha hiyo kwa darasa zima.

**Tathmini:** Bango lililokamilika lenye hatua tano za utatuzi wa tatizo, litakalowasilishwa mwishoni mwa darasa.

**Mpangilio wa Mazoezi:**

- **Utangulizi (Dakika: 5):**
  - Utaeleza kwa ufupi masuala ambayo wanafunzi wamechunguza katika masomo manne yaliyopita: fursa za upendeleo/utambulisho wa kibinafsi, pamoja na uhalisia na madhara ya matokeo ya ukosefu wa usawa katika viwango vya kijiji, kitaifa na kimataifa.
  - Baada ya wanafunzi kutaja baadhi ya masuala ambayo wamejadili, unapaswa kuandika nukuu hii ubaoni: "Usiwe na shaka kwamba kikundi kidogo cha wananchi wenye mawazo na kujitolea wanaweza kubadilisha ulimwengu; hakika, ndicho kitu pekee ambacho kimewahi kutokea." - Margaret Mead
  - Unapaswa kuwauliza wanafunzi wanafikiri dondoo hii ina maana gani, na kama wanadhani wanaweza kubadilisha ulimwengu (na kwa nini wanaweza au kwa nini hawawezi).

- **Maelekezo (Dakika: 5):**
  - Utaeleza wanafunzi kwamba leo, watakuwa wakichagua tatizo wanaloona katika jumuiya yao, na wataandaa orodha ya njia tano za kutatua matatizo hayo-inayoitwa "hatua za Utatuzi."
  - Unaweza kuchukua mapendekezo ya matatizo toka kwa wanafunzi, au ukawatajia mifano michache. Unaweza pia kuwapatia rundo la magazeti ya eneo mahalia ili wanafunzi waweze kuperuzi.

- **Kazi Binafsi (Dakika 25):**
  - Sehemu kubwa ya somo hili itajikita katika kuwapa wanafunzi muda wa kazi binafsi ambapo wanafunzi watachagua tatizo lao na hatua wanazoweza kuchukua kulitatua. Ikiwa wanafunzi wanataka kushughulikia tatizo moja linalofanana, wanaweza kufanya kazi pamoja katika vikundi vidogo.
  - Katika wakati huu, unapaswa kuzunguka darasani kila mara ili kuwasaidia wanafunzi kutambua masuala muhimu na kufikiria hatua za ubunifu. Unapaswa kuwahimiza wanafunzi kutumia uzoefu wao wenyewe katika jamii na pia kufikiria juu ya uwezo wao wakati wa kuunda hatua zao za utekelezaji (kwa mfano., mwanafunzi wa darasa la sita hawezi kuanzisha shirika lake, lakini anaweza kuchangisha pesa za kuchangia mashirika yaliyopo).

- Mwishoni, kila mwanafunzi/kikundi kinapaswa kuwa kimetengeneza bango dogo linalotaja tatizo wanaloshughulikia pamoja na hatua tano za utekelezaji. Ikiwa wana muda, wanafunzi wanaweza kupamba mabango kwa rangi, alama, stika, nk.

- **Mawasilisho (Dakika: 10)**
  - Kwa sehemu ya mwisho ya darasa, kila mwanafunzi atashirikisha darasa tatizo alilochagua na vipengele vyake vya kulitatua. Haya yanapaswa kuoneshwa ili wanafunzi wayaone, ili waweze kuhamasishwa daima kufanya kazi kwa manufaa ya jamii.